Jamhuri ya Kenya

Afisi ya Gavana
Serikali ya Ugatuzi ya Makueni

Hotuba ya Mheshimiwa Prof. Kivutha Kibwana, Gavana, Kaunti ya Makueni, Siku ya Madaraka, Tarehe Mosi Mwezi wa Sita Mwaka wa 2017

Wananchi wa Kaunti ya Makueni,

Waheshimiwa Viongozi Wateule wa Watu Wetu wa Makueni,

Wageni Waheshimiwa, Mabibi na Mabwana:

Siku ya leo tunasheherekea mpato wa kujitawala kama Taifa la Kenya. Tunawapa heko watu shupavu waliojitoa muhanga kupigania uhuru tunao ufurahia leo.

Tunafurahia kusheherekea ugatuzi na kujitawala ambako uhuru wetu umetuletea. Kama mnavyo kumbuka, mojawapo ya malengo ya ugatuzi kama ilivyowekwa katika kipengele cha 174 (c) cha Katiba ya Kenya (2010) ni kupeana mamlaka ya watu kujitawala na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika zoezi la mamlaka ya Serikali kwa kutoa maono juu ya mambo yanayo wahusu.

Tumejitahidi kuuweka msingi imara wa ugatuzi na kujiwezesha sisi wenyewe kujitawala hapa Makueni katika miaka 4 iliyopita. Tumeweka kipa umbele elimu juu ya malengo ya ugatuzi, na majukumu ya wananchi kupitia utaratibu wa mafundisho yanayohusu watu na serikali. Kwa hivyo tumeweza kuinua elimu ya watu wetu kujitambua kwa kiwango ambacho hakijawahi kuwepo hapo mbeleni katika nchi hii na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uongozi zaidi na pia kuchua majukumu ya uongozi wao. Ndio maana watu wa Makueni walikuwa wa kwanza kutuma maombi wakitaka serikali yao kusimamishwa kazi baada ya mafaragano yaliyotokea kati ya Kamati Tekelezi ya Kaunti na Bunge la Kaunti.

Nia ya kutaka kuwe na mpango mkubwa wa kuhamashisha wananchi uliyo na mikutano ya wananchi ya vijijini, mikutano ya wananchi ya vikundi vya kijijini, mikutano ya wananchi ya mitaa (Ward) midogo na mikutano ya wananchi ya Kaunti pamoja na kamati zao za maendeleo ilifuata baada ya utaratibu wa uelimishaji wa wananchi. Leo watu wetu wanashiriki katika majadiliano ya maendeleo wakichangia kuunda maisha yao ya baadaye kutoka kwa ngazi ya

vijiji hadi ngazi ya Kaunti. Uwajibikaji kwa umma pia umehakikishwa wakati wananchi wanashiriki katika shughuli za serikali na mipango mingineo kupitia kwa kamati za maendeleo.

Utawala wetu unaohakikisha mwongozo wa shughuli za serikali unaofaa una watawala 6 wa Kaunti ndogo, watawala 30 wa wadi na wengine 60 wa vijijini. Sasa tupo katika shughuli ya kuunda baraza za vijijini. Ni maoni yetu kwamba utawala wetu pamoja na mpangilio wetu mkuu tulionao wa kushirikisha wananchi unatuhakikishia serikali iliyo na ushirikiano, uwajibikaji na inayo weka wananchi mbele. Tunawahimiza nyote kushirikiana kikamilifu na mafisa hawa mnapo tafuta huduma na habari za mashauri ya uongozi, mipango na mipangilio ya serikali.

Tumetekeleza kwa uaminifu County Integrated Development Plan (CIDP) ya kuanzia mwaka wa 2013 hadi mwaka wa 2017 pamoja na blue print yetu ya maendeleo na Maono ya Kaunti ya Makueni ya mwaka wa 2025, ambayo yanalenga kupunguza umasikini kwa asilimia 30 kufikia mwaka huo. Ukaguzi wa mwisho wa CIDP ya mwaka wa 2013 hadi mwaka wa 2017 unaendelea kufanywa ukiangalia mafanikio, changa moto zilizo kuwemo na mambo tuliyo jifunza. Shughuli hii inasaidia kuundwa kwa CIDP ya mwaka wa 2018 hadi mwaka wa 2022.

Tumeikaribisha Secretariat ya Public Expenditure na Financial Accountability (PEFA) ya Benki ya Dunia, ikishirikiana na Kenya Institute for Public Policy and Analysis (KIPPRA) kufanya ukaguzi wa matumizi ya pesa za umma wa kina, wa kila mara na wenye ushahidi. Ukaguzi huu unapima jinsi utaratibu wa matumizi ya pesa za umma, utendaji na mashirika zinavyo changia matokeo ya bajeti yanayo pendeza. Ukaguzi huu unalenga mambo yafuatayo yakiwemo matumizi ya pesa za umma, bajeti ya kuaminika, uwazi katika pesa za umma, usimamizi wa rasilimali na madeni, policy based fiscal strategy na kupanga bajeti, ubashiri na usimamizi wa utekelezaji wa bajeti, makadirio ya hesabu na kutoa ripoti, uchunguzi wa nje na utathmini na utoaji wa huduma bora.Tunawahakikishia wananchi wetu ya kwamba matokeo hayo na mapendekezo ya uchunguzi huu yatatekelezwa kwa maana yanatujulisha juu ya mipangilio yetu ya ndani na hazina ya Kaunti.

Ndugu zanguni:

Katika kufanikisha maono yetu ya pamoja ya kuwa na kaunti yenye mafanikio pamoja na maisha ya hali ya juu tayari tuko mbele. Sisi ndio Kaunti ya kwanza kutekekeleza na kufanikisha matibabu kwa wote baada ya kufanya majaribio ya watu wenye miaka 65 na kwenda juu. Sasa wakaazi wanapata matibabu ya bure katika zahanati na hospitali zetu baada ya uandikishaji wa lazima kila nyumba. Hili jambo limepunguza mategemeo ya harambee za kulipia wagonjwa hospitali. Tunawahakikishia watu wetu kwamba tumejitolea kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya kwa wote kulingana na viwango vilivyowekwa na World Health Organization (WHO).

Pia, tumeandaa Makueni County Climate Change Fund Regulations, 2015 ambazo zilipitishwa na Bunge la Kaunti ili kuweka msingi wa kuzuia hadhari za mabadiliko ya hewa na pia kukusanya rasilimali za kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa. Miradi kumi (10) tayari imeshafanywa katika Wadi sita kwa kutumia huu mfuko. Hili limetendeka kwa kushirikiana na Anglican Development Services Eastern (ADSE).

Sisi ndio kaunti ya kwanza kuanzisha huduma iliyojitosheleza ya kushauri watu (counseling services unit) ambayo ina washauri (Counsellors) 10 anaotoa huduma za ushauri na kepeana psycho-social support kwa wafanyikazi na watu wetu katika kaunti ndogo sita (6). Kuanzia Septemba mwaka wa 2016 hadi Mei mwaka wa 2017, washauri hawa wameweza kuhudumia watu 57,435 ambao walihitaji huduma mbali mbali.

Sisi pia ndio kaunti ya kwanza kuanzisha kuweka vifaa katika maktaba 30 katika shule za msingi tukishirikiana na watu wengine. Tungependa kuimarisha utamaduni wa kusoma vitabu ambao utachangia kuboresha matokeo ambayo kaunti yetu inatambulika kwayo.

Mpangilio wetu wa kushauri na kuongoza watoto wetu wanaomaliza kidato cha nne umefikia zaidi ya vijana 10,800 kwenye miaka miwili na niwa kipekee katika nchi yetu. Mpango huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Shina Foundation na unafundisha mambo yafuatayo na mengineo: kujielewa, kuchagua namna ya maisha, ufanyi biashara, madawa ya kulevya, kufanikisha afya ya watoto wa kike wakati wa hedhi, ushauri na michezo na ukuzaji wa talanta.

Sisi ni mojawapo wa kaunti za kwanza zilizo anzisha kamati ya utathimini ya kaunti kwa kufuatia matakwa ya Public Finance Management Act, 2012 na Public Finance Management Regulations, 2015.

Mabibi na Mabwana:

Nikubalieni kuwaeleze kwa ufupi mafanikio mengine ya miaka 4 ambayo imepita:

Katika Elimu tumewaajiri waalimu 900 wa shule za chekechea na wakufunzi 129 wa County Technical Training Institutes (CTTI). Tumepeana pia zaidi ya scholarships 104 kwa vijana ili waweze kupata masomo ya sekondari. Zaidi ya wanafunzi 2000 wa secondari, colleges, CTTI na vyuo vikuu wemetunukiwa bursaries.

Sehemu 16 za kutoa habari kwa umma zimeanzishwa na zinafanya kazi. Shule 113 za chekechea zimejengwa na kuwekwa viti 42,000 vya watoto. Matangi 240 ya kuhifadhia maji yamepeanwa kwa shule za chekechea na pia shule 240 za chekechea zimepewa vifaa vya michezo.

Katika sekta ya afya, mafanikio makubwa yameonekana, mengineo yakiwa ni: madaktari maalum wameongezeka kutoka 7 mwaka wa 2013 hadi 12 mwaka wa 2017. Maafisa wa Afya wameongezeka kutoka 36 mwaka wa 2013 hadi 61 mwaka wa 2017. Wahudumu pia wameongezeka kutoka 440 mwaka wa 2013 hadi 663 mwaka wa 2017. Madaktari wa meno wameongezeka kutoka 3 mwaka wa 2013 hadi 9 mwaka wa 2017 na Pharmacists wameongezeka kutoka 9 mwaka wa 2013 hadi 12 mwaka wa 2017. Pharmaceutical Technologists wako 22 na Emergency Medical Technicians (EMTs) 13 pia wameajiriwa kuimarisha huduma katika sekta ya afya.

Serikali imeboresha sehemu za utoaji huduma za afya kwa kununua vifaa vya matibabu. Imefanya idara ya radiology ya hospitali ya Mbooni iwe ya kisasa na ikanunua ambulance 15 za kaunti ambazo zimesaidia pakubwa katika upatikanaji wa matibabu ya dharura.

Pia tumejenga vyumba vya upasuaji (theatre) kwenye hospitali za kaunti ndogo za Tawa, Makindu, Kilungu na Kibwezi na pia huko Sultan Hamud. Genereta pia zimenunuliwa kuhakikisha vyumba vya upasuaji (theatres) vinafanya kazi hata wakati umeme umekatika.

Kituo cha kuwahudumia watu ambao wamepata mishtuko (trauma) kimeanzishwa hospitali ya kuanti ya Makindu na pia kituo cha mawasiliano ya ambulance kimeanzishwa hapo. Vyumba vya X-Ray vimejengwa katika hospitali za Sultan Hamud na Kaunti ndogo ya Kilungu.

Marekebisho yalifanywa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Makueni Kaunti na pia huduma za afya kwa mama na watoto zikaanzishwa hapo. Pia tumefanya marekebisho kwenye vituo vya matibabu katika kaunti nzima na tukajenga vyumba vya akina mama kujifungulia.

Katika sekta ya maji tunapanga kuhakikisha ukusanyaji wa maji ya mvua kwa kiwango kikubwa katika kaunti yote. Kuwezesha hili, tayari tumenunua mashine 1 ya kuchimba maji, malori 6 ya tipper, excavator 3 na dozer 1. Pia tumenunua vifaa vya kupima maji katika ardhi na mashine za kibiologia za kupima maji na madawa ya kusafisha maji kwa matumizi ya binadamu. Visima vipya vya maji vimechimbwa na pia tumerekebisha zaidi ya miradi 14 ya maji na kuifanya itumike. Mabwawa 88 yamechimbwa ilhali mengine 27 yanaendelea kuchimbwa.

Mabwawa yafuatayo kati ya mengine yamemalizika: Kwa Mbila Earth Dam, Kwa Ndulu Earth Dam, Kwa Luma Earth Dam, Kwa Kalii Earth Dam, Mukulu Earth Dam, Mwea Earth Dam, Ngaamba Earth Dam, Kwa Kakui Earth Dam na Kulumbus Dam ambayo inakaribia kuisha. Miradi ya unyunyiziaji maji 6 imeanzishwa huko Mwinzeni, Kilome, Kithalu, Kikuu, Luani, Yathonza, Muiu na Sikika na pia mabwawa 96 yamechimbwa.

Idara ya Vijana imefaulu kupanga mara mbili mashindano ya mbio za masafa marefu ambazo zimehudhuriwa na wakambiaji kadhaa wa kimataifa. Idara hii tayari imesawazisha na kujenga magoli kwenye viwanja 22 katika kaunti. Serikali imefadhili na kuwezesha makundi kwa vifaa kama vile matangi ya maji, green houses, drip irrigation kits, mahema na viti ili kuimarisha mambo yao yakiuchumi yanayoendelea. Vikundi 6 vimesaidiwa na drip irrigation kits na kikundi kimoja kikasaidiwa na mashine ya kuosha gari. Vikundi 3 vimesaidiwa na mbuzi 14 wa maziwa, vikundi 2 vimepokea green houses, vikundi 18 vya kujisaidia na makundi ya jamii yafadhiliwa na mahema ya kukaa watu 100 pamoja na viti; vikundi 37 vimefadhiliwa na matangi ya maji ya lita 5000. Matangi 300 yamegawanywa kupitia mpangilio wa '*Nzangule ya Matangi'*.

Zaidi ya wanabiashara 5100 wamepata mafunzo ya kibiashara. Kupitia kwa *Tetheka* Fund. Makundi 136 ya walemavu na makundi mengine 640 yamepewa mikopo ya dhamani ya shilingi ya Kenya 43,260,000.

Kitengo cha Jinsia kimewezesha ukugazi na uandikishaji wa watu zaidi ya 4,230 wenye ulemavu. Na pia kilisaidia zaidi ya watu 150 wenye ulemavu kwa vifaa vya kujisaidia na wengine139 wenye ulemavu wakasaidiwa kupata miguu na mikono bandia na viti vya magurudumu kutoka Jaipur Trust. Mashirika 8 ya watu walemavu yalisaidiwa na matangi ya lita 5000 ya kukingia maji ya mvua na mashirika mengine14 yakasaidiwa na green houses.

Kumbi 9 za kijamii zimejengwa na kumalizika na zingine 4 zinaendelea kujengwa. Zaidi ya wasichana 5300 kwenye kaunti wamepata psycho-social support na sodo (sanitary towels) na zaidi ya vijana 350 wemepata nafasi za intership na kazi za kujitolea kutumikia serikali.

Katika idara ya Ardhi, zaidi ya vyeti 5000 vya kumiliki mashamba vilipeanwa Kyuu, Yandue, Uvete, Kai A, Syumile, Mbui Nzau na Kisingo. Zaidi ya faili 700 za cadastral survey zimekabidhiwa mkuu wa survey ili atoe vyeti vya kumiliki mashamba. Plani za majengo ya masoko 98 zimekamilishwa na mipango ya maendeleo ya Wote, Sultan Hamud, Mtito Andei, Ukia na Mukuyuni imetimizwa.

Idara ya Barabara, Usafiri na Miundo Msingi imenunua vifaa vya kujenga barabara ambavyo ni grader 2, backhoes2, roller 2 na tipper 3. Barabara mpya zaidi ya 1400 zimefunguliwa na pia kilomita 1,629 za barabara zimelimwa kwa wepesi na kwa uzito. Zaidi ya kilomita 200 za barabara zimwekwa marrum na zaidi ya kilomita 0.6 ya barabara imewekwa cabro Wote town.

Katika maendeleo ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi, mtazamo mkubwa uko upande wa ukulima wa matunda na mboga. Hiki ni kilimo cha dengu, mbaazi, dolichos, njegere na maharagwe. Idara hii inalenga nafasi kubwa iliyoko ya unyunyiziaji pamoja na ukulima wa maziwa, ufugaji wa kuku na ng'ombe na mbuzi wa nyama. Kwa sasa serikali imeanzisha mifano ya viwanda vya kwanza vitatu: kimoja ni cha kuongezea thamani ya matunda kinachoitwa Kalamba Fruit Processing Plant, mradi wa maziwa ambao umewezesha kuwekwa kwa vikundi vya ukulima wa maziwa, ununuzi wa mashine 8 za kuhifadhi maziwa yasigande kwa cooperative 8, mtambo mdogo wa kutengeneza maziwa huko Kikima, piki piki 2 na pickup 2 na uzalishaji kwa njia ya mpira wa bei nafuu ili kuongezea ubora wa ng'ombe na wingi wa maziwa. Idara hii tayari imesha pachika mimba ng'ombe 10,000 kwa njia hii ya mpira. Mpango wa Kaunti wa kuimarisha kilimo cha maziwa tayari unaendelea. Idara hii imechagua mafundisho bora ya ukulima wa maziwa na tayari wakufunzi wamesha tumwa hadi kwenye kiwango kidogo cha lokesheni kwa dhamani ya shilingi milioni 7.5 ya Kenya. Kalamba Fruit Processing Plant itafunguliwa hivi karibuni.

Waheshimiwa Mabibi na Mabwana:

Kulingana na Maono ya Kaunti ya Makueni ya mwaka wa 2025, tumetenga shilingi bilioni 1 ya Kenya kwa miradi ya maji katika bajeti ya mwaka ujao. Matumizi sitiri ya rasilmali ya maji haya kupitia unyunyizaji mdogo mdogo yatachangia kupunguza umasikini kwenye kaunti. Pia tumetenga shilingi milioni 80 ya Kenya kwa maendeleo ya miji kenye bajeti ya mwaka wa 2017/2018. Kuendelea kwa miji kunahitaji kuchochea maendeleo sitiri kwenye miji yetu ili kuwezesha maendeleo ya uchumi yanayo wawezesha wananchi kujichumia mali. Hii ni baadhi ya mipango iliyoko ya kuimarisha maendeleo ya ugatuzi kwenye mwaka ujao.

Katika siku 67 zijazo tutakuwa na uchaguzi mkuu nchini Kenya. Ninawaomba nyote mtembelee vituo vyovyote vya kupigia kura vilivyo kwenye Wadi zenu ili kuthibitisha kama mmeandikishwa kupiga kura. Kumbukeni kubeba vitambulisho au pasipoti zenu. Zoezi hili litamalizika tarehe 9 mwezi wa June na ni muhimu kuhakikisha utaweza kupiga kura kwenye uchaguzi ujao.

Katika kipindi cha kampeni, tunawahimiza kutimiza haki zenu za kidemokrasia kwa njia ya amani na utulivu. Tunawaomba wagombeaji wote wa viti vya kisiasa wazifanye kampeni zao kwa heshima.

Tumeweka misingi ya ugatuzi na kuongeza kina cha kujitawala hapa Makueni kwenye miaka 4 iliyopita. Sasa tuna tafuta kuimarisha faida za ugatuzi na tuna tazamia mapendeleo yenu mema wakati wa uchaguzi. Tunawaomba mfanye uamuzi wa hekima mnapo piga kura zenu tarehe 8 mwezi wa Agosti 2017.

Ninawatakia ndugu zetu wote wa Kiislamu mwezi mtakatifu wa Ramadhan. Nina watakia nyote Siku ya Madaraka yenye furaha.

Nina washukuru nyote kwa kunisikiliza.

Kivutha Kibwana
Gavana